

Biblia inasemaje....

Yesu aliyachukuliaje maandiko?

Sehemu ya tatu

“Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi” Mathayo 12:40.

“Na kama ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika siku zake mwana wa Adamu. Walikuwa wakila na kunywa, walikuwa wakioa na kuolewa, hata siku ile Nuhu aliyolingia katika safina, gharika ikashuka ikawaangamiza wote,” Luka 17:26-27.

Katika kujifunza namna Yesu alivyoyachukulia maandiko nyakati zake, ni dhahiri kwamba Yesu alijua kuwa maandiko ni ya kweli, na kwamba yaliandikwa ili tujifunze. Hata Paulo naye alituambia katika Warumi 15:4,

“Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini”

Ukosoaji wa leo, una lengo la kuharibu ujumbe wote mzuri ambao unatokana na Agano la Kale, kwa kule kusema kuwa Yona na nyangumi ni hadithi tu. Na kwamba gharika ilifunika eneo dogo tu na siyo ulimwengu wote. Walakini, Yesu aliye Mwana wa Mungu, aliyekuwako tangu kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu huu, aliwaambia wanadamu kuwa habari ya Yona na Nuhu ni kweli. Bila shaka yoyote, Yesu alibainisha kuwa angezikwa katika ardhi kwa siku tatu kama Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi. Pasipo shaka yoyote, Yesu alipokuwa anazungumzia ujio wake wa pili, alifananisha na jinsi matukio yalivyokuwa siku za Nuhu ili kuonyesha kuwa Mtukio ya gharika yalikuwa ni matukio ya kweli, ambapo gharika “ikawaangamiza wote,” Luka 17:26-27

Yesu, aliye Bwana wetu, alijua kuwa habari za Agano la Kale ni za kweli. Leo, kama wanadamu, nasi vivyo hivyo tunatakiwa kuamini alichokijua Yesu. Kusadiki kisichoonekana kwa ushahidi ulio katika maandiko, hiyo

ndiyo imani, Waebrania 11:1. Katika mafundisho yake, Yesu alionyesha kuwa Agano la Kale ni la kweli; Sasa, na wewe unasadiki kwamba ni la kweli? Waebrania 11:6.